**HOTUBA YA MGENI RASMI MWENYEKITI WA BODI YA USHAURI YA MAMLAKA YA HALI YA HEWA DKT BURUHANI NYENZI KATIKA UFUNGUZI WA MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA MAMLAKA YA HALI YA HEWA KATIKA UKUMBI WA UDBS CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM. TAREHE 30/3/2016 SAA NNE ASUBUHI.**

Mwenyekiti wa Baraza na Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dkt. Agnes Kijazi

Wakurugenzi na Mameneja wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,

Wawakilishi wa TUGHE Taifa,

Mwenyekiti wa TUGHE – TMA,

Viongozi wa Matawi ya TUGHE - TMA,

Wajumbe wa Baraza la wafanyakazi la Mamlaka ya Hali ya Hewa,

Wanahabari,

Wageni waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwepo hapa leo hii tukiwa na afya njema. Pia nikushukuru Mwenyekiti wa Baraza pamoja na timu yako kwa kunipa heshima ya kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa Baraza la wafanyakazi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa.

**Ndugu Mwenyekiti na wajumbe wa Baraza,**

Kama ulivyotangulia kusema ndugu Mwenyekiti wa baraza kuwa Baraza hili limehudhuriwa na viongozi wa Mamlaka, wawakilishi wa wafanyakazi kutoka katika vituo vyenu mbalimbali hapa  nchini kwa kuzingatia muundo wa mkataba wa baraza, nimefurahi kwamba mnatekeleza mkatiba huo kama mlivyokubaliana kati ya uongozi na wafanyakazi.

Aidha, napenda kuchukuwa fursa hii kuwapongeza wajumbe wote wa Baraza kwa kutenga muda ili kuhudhuria kikao hiki cha Baraza. Nafahamu kwa upande wenu mnachapa kazi kwa saa ishirini na nne hivyo kutenga muda wa kukutana kwaajili ya shughuli za Baraza ni jambo linalostahili pongezi. Siku hizi teknolojia imeendelea na ninavyofahamu TMA mko mbele katika masuala ya Teknolojia hivyo mngeweza kuufanya mkutano huu hata kwa njia ya Video Conference lakini mmeona vyema mkutane ili kuwa na

majadiliano ya kina kwa njia ya ana kwa ana. Nawapongeza sana kwa uamuzi huo.

**Mwenyekiti wa baraza, wajumbe wa baraza, mabibi na mabwana.**

Hata kama kutakuwa na Sera, Sheria na Kanuni nzuri katika mahali pa kazi pasipokuwa na ushirikiano baina ya mwajiri na watumishi itakuwa vigumu Taasisi kutimiza malengo yake. Hivyo pamoja na mambo mengine, Baraza hili lina wajibu wa kuishauri Mamlaka kwa lengo la kuleta tija na mshikamano baina ya mtumishi na mwajiri. Ni vyema madai ya maslahi ya watumishi yaendane na kiwango cha utekelezaji wa wajibu wao, kwa maana hiyo hakuna haki bila ya wajibu. Nichukue fursa hii kuwakumbusha watumishi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa kutekeleza majukumu yenu ya kazi kwa kuzingatia kanuni na taratibu za kazi. Hakikisha unatekeleza wajibu wako ndipo uwe kwenye nafasi nzuri ya kudai maslahi yako. Na kwa upande wa mwajiri mtumishi anayetekeleza majukumu yake apatiwe stahili zake na pale anapostahili pongezi apongezwe. Lakini kwa yule ambaye hatekelezi majukumu yake hatua za nidhamu zichukuliwe dhidi yake kulingana na taratibu zilizopo ili kuhakikisha watumishi wote mnafanyakazi kama timu kama mlivyoeleza katika thamani kuu (Core Value) za

Mamlaka. Hii itaiwezesha Mamlaka kutekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya serikali ya awamu ya Tano ya HAPA KAZI TU. Bodi ya Ushauri ya Mamlaka ya Hali ya Hewa itafurahi kumpongeza mtumishi mbunifu anayesaidia Taasisi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi lakini pia haitamfumbia macho mtumishi yeyote mzembe asiyetimiza wajibu wake.

**Mwenyekiti wa Baraza, Wajumbe wa Baraza, Mabibi na mabwana;**

Napenda kuchukuwa nafasi hii kuwapongeza watumishi wote wa Mamlaka ya Hali ya Hewa chini ya uongozi wako Mwenyekiti kwa kuweza kutekeleza majukumu mliyopewa kitaifa kwa ufanisi Mkubwa. Sisi tuko karibu na wananchi na tunasikia wanavyoizungumza Mamlaka. Wengi wameongeza imani kwa huduma mnazotoa na hii ni kwasababu viwango vya usahihi wa utabiri mnaotoa vimeendelea kuongezeka kwa kiwango kikubwa.

Nafahamu kwamba mnazo changamoto nyingi ikiwemo, Jengo kwa ajili ya kituo kikuu cha utabiri, mtandao wa vituo vya uangazi ambao hautoshelezi mahitaji, Sera ya Taifa ya hali ya hewa ambayo bado inaandaliwa, ufinyu wa bajeti ambayo haikidhi mahitaji halisi ya uendeshaji wa vituo ya Hali ya Hewa nchini na

maslahi ya wafanyakazi. Pamoja na changamoto hizo bado mmeweza kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi ikiwemo kuendelea kumiliki cheti cha kimataifa katika utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa sekta ya usafiri wa anga, kuendeleza wafanyakazi kitaaluma, kutoa utabiri na tahadhari juu ya matukio ya hali mbaya ya hewa kwa wakati pamoja na mengine mengi. Kwa kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi mmechangia katika kuokoa maisha ya watu na mali zao.

Aidha, Bodi ya Ushauri inapenda kuishukuru serikali kwamba pamoja na changamoto ya ufinyu wa bajeti katika serikali kwa ujumla wake bado serikali kwa kutambua mchango wa sekta ya hali ya hewa nchini inaendelea kuboresha miundombinu ya hali ya hewa ikiwemo vituo vya uangazi, vifaa, rada za hali ya hewa na ujenzi wa kituo kikuu cha utabiri ambacho kwa muda mrefu serikali imekuwa ikigharamia kukodi.

**Ndugu Wajmbe wa Baraza;**

Ni ukweli usiopingika kwamba kiongozi bora si yule anayejisifia kuongoza sehemu isiyokuwa na changamoto, bali ni mtu mbunifu, anayeweza kuongoza wakati kunapokuwa na changamoto na anatakiwa aone mbali zaidi ya wengine na kabla ya wengine.

Kwa upande menejimenti ya Mamlaka ya Hali ya Hewa chini ya Uongozi mahiri wa Mkurugenzi Mkuu Dkt Agnes Kijazi sifa hizo za uongozi na za kiutendaji mnazo ndiyo maana mmepewa dhamana kubwa ya kusimamia na kutekeleza shughuli za serikali kwenye vituo vyenu viliyopo mikoani pamoja na Makao Makuu. Na ndio sababu watumishi wengi wa Mamlaka mko katika vikosi kazi mbali mbali vya kimataifa chini ya Shirika la Hali ya Hewa Dunia. Na pia Mkurugenzi Mkuu Dkt. Agnes Kijazi ni mjumbe katika Mjumbe kamati kuu ya utendaji "Executive Council" kwa kipindi cha 2015 hadi 2019. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri mnayofanya na nitumaini la Bodi ya Ushauri kuwa mtaendelea kufanya vizuri zaidi ya hapo.

**Ndugu Mwenyekiti na wajumbe wa Baraza, Mabibi na Mabwana;**

Nimejulishwa kuwa Katika kikao hiki, mada mbali mbali zitawasilishwa kwa utaratibu shirikishi ikiwemo ya maadili ya utumishi wa umma. Ni matumaini yangu kuwa baada ya kikao hiki, mtazingatia maudhui ya mada zote zitakazowasilishwa na kuzitumia katika kuboresha utendaji katika maeneo yenu ya kazi na Mamlaka kwa ujumla. Aidha nimejulishwa kwamba

mada kuu ya Baraza hili ni kupitia Bajeti ya Mamlaka kwa mwaka 2016/17. Natumaini mtakuwa makini kuweka vipaumbele sahihi ili kuhakikisha mafanikio mliyofikia yanazidi kuboreshwa. Baada ya kupata mafanikio msibweteke bali mzidi kuwa wabunifu ili mboreshe zaidi. Mmesema viwango vya usahihi wa Utabiri ni zaidi ya asilimia 80, wekeni vipaumbele sahihi katika bajeti ili viwango hivyo vizidi kuongezeka

**Ndugu Mwenyekiti wa Baraza;**

Napenda kumalizia hotuba yangu kwa kukumbushana kuhusu janga la **UKIMWI**. Nchi yetu imekuwa ikipoteza nguvu kazi kwa kiwango kikubwa kutokana na janga la ugonjwa huu**.** Nachukua fursa hii kuwaasa wana TMA kuchukua tahadhari na wale ambao tayari wameathirika kufuata ushauri wa madaktari ili kuhakikisha mnaendelea kuwa na afya njema. **Mamlaka ya Hali ya Hewa bila ukimwi inawezekana.**

Mwisho, nihitimishe kwa kuwatakia kikao chenye mafanikio yaliyokusudiwa. Ni matarajio ya Bodi ya Ushauri kwamba mtahitimisha kikao hiki kwa maazimio yatakayowawezesha kufanya kazi kwa bidii na uadilifu. Ni heshima yangu kutamka kwamba

**‘MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA MAMLAKA YA HALI YA HEWA’ Umefunguliwa Rasmi**

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA.**